# HADISI YA N’IBAMBA DOUCE NAMWEZI



N'Ibamba alizaliwa tarehe kumi na moja mwezi wa pili wa mwaka 1989 pa Bukavu, muji ambao una kuwa pembeni ya ziwa kivu.

Bukavu ni muji mkuu wa jimbo la Kivu ya Kusini, katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Wazazi wake wote ni wakongomani na ni waganga, wana ishi incini umo na wame zaa wazozo munane, Douce ni mutoto wa pili wa watoto wanane hao.

Alipokuwa na umri wa miaka minane, familia yake ililazimishwa kukimbia makazi yao na kuishi na watu wengine ambao walikuwa wamehamishwa kwa muda fulani, kufuatia vita vya wenyewe kwa wenyewe vya kupata mamlaka.

Alisoma katika chuo cha Alfajiri na kisha akapata diploma ya mahusiano ya kimataifa katika chuo kikuu cha Bukavu ama UOB. Kuanzia umri mdogo, N'Ibamba alitaka kuwa mwandishi wa habari, lakini watu wengi walimwambia kuwa haikuwa kazi ya wanawake.

Hata hivyo, alikaziya ndoto yake, alianza kutayarisha vipindi vya redio akiwa na umri wa miaka kumi na sita katika kituo cha redio cha Kikatoliki, Radio Maria, na miaka mbili baadaye alijiunga na Chama cha  Femmes des Médias du Sud Kivu (AFEM) ama muungano ya wanawake wanao kuwa wahariri.

Wakati huo, DRC ilikuwa katika vita na N'Ibamba alishiriki kwenye rekodi la hadisi hewani za wanajeshi watoto wa zamani na ubakaji mkubwa ambao uli kuwa ndani ya tarafa za jimbo. Baada ya miaka 10 kama mufanya kazi wa AFEM , aka chukua na fasi ya musimamizi kwa muda wa uongozi wa AFEM

## HADISI YA N'IBAMBA DOUCE NAMWEZI

Mu mwaka wa 2016, N'Ibamba alikuwa msimamizi wa vipindi katika redio ya AFEM iitwayo MAMA Radio. Kituo hico cha redio kili undwa kwaku inuwa usawa wa kijinsia kati ya wanawake na wanaume.

Munamo mwaka wa 2018, aliondoka MAMA Radio na kuanzisha shirika lake mupia linalo itwa Uwezo Afrika Initiative. Kampuni hiyo ina kuwa bila faida na ina kuwa na lengo ya kupiganisha vitu ambavio havi semeke wazi ndani ya jamii na ku shauriya vijana binti na wana wake ku husu usafi wa mwili zao hasa wakati wa damu ya mwezi .




Hii inafanyika kupitia uandishi wa habari, mafunzo ya ufundi na namuna gani mwanamuke ana weza kuji tumainiya kifeza mwenyewe. Pia UWEZO Afrika una gabula vifaa vya afya ya ngono na usafi wa mwili wa wanawake katika inci, katita vifaa vile kuna kuwa nguo zina tengenezwa kwaku tumikishiwa zidi ya mara pili wakati wa damu ya mwezi na vina weza ku fuliwa.

Munamo mwaka 2020, N'ibamba Douce ame ungana na miungano sita ya kitamaduni katika muji la Bukavu, pamoja wame anzisha Nafasi ya Kitamaduni inayo itwa Espace culturel KWETU ART ama ECKA , na Douce ana kuwa na fasi ya mwenyekiti wa kamati ya uongozi.

Katika hiyo tuu mwaka wa 2020, alitajwa na BBC katika oroza yake ya kila mwaka ya wanawake wenye ushawishi mkubwa zaidi wa mwaka 9,10.

Makala ya Uwezo Afrika ime tu ambiya mambo yafwatayo ku husu N'ibamba Douce:

## HADISI YA N’IBAMBA DOUCE NAMWEZI

“*BBC imeonesha oroza yake ya Wanawake 100 Wenye Msukumo na Ushawishi Ulimwenguni kote kwa 2020. Wanawake 100 wa mwaka huu wanaangazia wale wanaoongoza mabadiliko na kuleta mabadiliko katika nyakati hizi za misukosuko.*

*Oroza ya BBC inajumuisha Sanna Marin, anayeongoza serikali ya muungano ya wanawake wote wa Finland, Michelle Yeoh, nyota wa filamu mpya za Avatar na Marvel na Sarah Gilbert, anayeongoza utafiti wa Chuo Kikuu cha Oxford kuhusu chanjo dhidi ya virusi vya corona, pamoja na Jane Fonda, hali ya hewa. mwanaharakati na mwigizaji. Douce Namwezi N'Ibamba ndiye mwanamke pekee kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwenye orodha hii ya wanawake 100 wenye ushawishi duniani.*

*Douce Namwezi N'Ibamba ni mwandishi wa habari wa vyombo vingi vya habari na mwanzilishi wa Uwezo Afrika Initiative, shirika lisilo la faida linalokuza uwezeshaji wa wanawake kupitia uandishi wa habari, mafunzo ya ujuzi na ujasiriamali wa kijamii. Inapigana na miiko kuhusu hedhi kwa kuwapa wanafunzi na wanawake katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo elimu ya ngono na vifaa vya usafi.*

*Makala lile la Uwezo Afrika unatu julisha ya kuwa Douce Namwezi ali unda vikundi viitwavio timu Maisha katika shule tatu mujini Bukavu. Lengo ya vikundi vile niku zungumuza ku husu usafi wa wanawake hasa wakati wao wa damu ya mwezi na namna gani kutumikisha nguo zinazo tengenezwa ka ajili ya ma binti wakati ule. Wanafunzi wa binti  wanapokea kila mumoja paketi ya vifaa via Maisha Pad zilizotengenezwa na Uwezo Afrika Initiative.*

*Douce Namwezi N'Ibamba ame pata ndoto zake zaku saidiya jamii ku pitiya utambulisho wa mama yake Claudine Namwezi na babake Lambert NIbamba kama vile waganga. Jina likiwa ni ishara, kanzu nyeupe za waganga hawa wawili humutia moyo kwa usafi*.

*Gazeti la Carrefour des enfants du Congo (Careco) linamfundisha kuhusu mashindano ya ubunge. Chuo Kikuu cha Bukavu (Uob) kinamfundisha ku cambuwa hali ya maisha. Mama Radio ikamupa na fasi yaku cora sauti yake kama muhariri.*

*Douce Namwezi bado haja maliza ku fikiriya ku husu namna gani yaku saidiya jamii yake ku songa mbele na hasa inci lake. Ana ndoto ya kukuza zaidi haki za wanawake na upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi kwa wanawake”*.

N’ibamba Douce ame kuwa piya mjumbe wa kamati ya maandalizi la toleo la kenda la Tamasha la Amani ama festival amani iliyo pitika mujini mara ya kwanza pa bukavu munao mwezi ya pili mwaka wa 2023.

Douce ame fasiriya ya kwamba ili kuwa muradi nzuri waku leta toleo lile mujini Bukavu na ime saidiya ku onesha ya kuwa muji wa bukavu ina kuwa na wataalamu wengi ambao wana piganiya maendeleo na Amani juu ya inci ya Kongo.

Tukilingana na redio okapi tuna soma misemwa hii ya Douce katita tamasha lile: *“ Siku hizi tatu zilitoa jiji la Bukavu wakati wa mshikamano wa kijamii kama tamasha la Amani lilivyotaka. Watu*

## HADISI YA N’IBAMBA DOUCE NAMWEZI

*kutoka asili tofauti na wasifu tofauti, vijana, wazee, watoto walipata nafasi yao wenyewe, waliweza kushiriki, licha ya hali mbaya ya hewa. Kwa hivyo kwangu ilikuwa mafanikio."*

Kwa Leo N’ibamba iko mama wa watoto tatu ame funga ndowa na Bwana Placide Ntole ambaye ana kuwa mutete wa hazi za binaadamu na piya mwanasheria mujini Bukavu.

Mu mwaka wa 2021 N’ibamba na mume wake wame tembeza toleo ya pili ya Requiem for peace na niku pitiya shirika uwezo Afrika ndiyo ile toleo ime endeshwa mujini bukavu.




Lengo la toleo lile ni kudai haki itendeke kwa kumbukumbu ya wahanga wa moja kwa moja na wasio wa moja kwa moja wa vita na mauaji nchini DRC. Pia inataka ku unga mukono mshikamano wa kijamii, upatanisho kati ya wahasiriwa na wahalifu kupitia ukweli, upatanisho na haki. Baada ya Bukavu, shughuli hiyohiyo ili endeleya pa Goma, kisha Kinshasa, kwa usaidizi sawa na Ushirikiano wa Uswizi.